TANGAZO LA SERIKALI NA. 909 la tarehe 16/10/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

------------------

# SHERIA NDOGO

------------------

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2020

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

*"ada"* maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali, au leseni zitolewazo na Halmashauri;

"*Afisa Mwidhiniwa*" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"*chombo cha usafiri"* maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa

mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo;

"*Halmashauri*" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya;

"*kibali*" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri ;

"*machinjio*" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"*madini ya ujenzi*" maana yake ni mchanga, mawe, kokoto, udongo, matofali ya kuchoma au mabichi na chokaa ;

"*maegesho*" maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

"*mhudumu*" maana yake ni mtu yeyote anayehudumia wateja katika eneo la biashara;

"*Mkurugenzi*" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya pamoja au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"*usajili wa vyombo vya usafiri*" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri;

"*ushuru*" maana yake ni malipo yanayofanywa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma inayotolewa na Halmashauri;

"*ramani ya jengo*" maana yake ni mchoro au michoro

inayotakiwa kuwasilishwa Halmashauri chini ya Kanuni za udhibiti wa maendeleo ya Ujenzi Mijini;

"*soko*" maana yake ni sehemu yoyote maalum iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa;

"*Wakala*" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni au Asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri ;

## SEHEMU YA PILI
## NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa au wakati wa kupata huduma au baada ya kupata huduma.

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na Ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni-

(a) huduma za Ardhi;

(b) kukodi magari na Mitambo ya Halmashauri;

(c) upimaji wa Afya;

(d) uwekaji wa uzio kwenye eneo la ujenzi;

(e) machinjio;

(f) kulaza mifugo;

(g) ukaguzi wa afya ya mnyama kabla ya kuchinjwa;

(h) ukaguzi wa mnyama kuruhusu kwenda buchani;

(i) kuruhusu kuingiza wanyama na nyama iliyochinjwa nje ya Halmashauri;

(j) huduma nyingine zinazohusu mifugo;

(k) madini ya ujenzi;

(l) stendi;

(m) burudani na michezo;

(n) mazao ya kilimo na biashara;

(o) mazao ya Misitu;

(p) uondoaji wa maji taka;

(q) huduma nyingine;

(r) maegesho kwenye maeneo maalum;

(s) kuosha magari (Car Wash)

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5. (1) Itakuwa ni Wajibu wa kila Mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya Ushuru utakuwa ni kwa masaa yote ishirini na nne (24).

(3) Malipo ya Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na Mlipa Ushuru.

(4) Malipo ya Ushuru yanayotozwa kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya Halmshauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Mabadiliko ya Viwango vya ada na ushuru

6. (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho ya viwango vya Ada na Ushuru pale itakapoona inafaa.

Sura 288

(2) Katika kufanya marekebisho ya viwango vya Ada na Ushuru au kipengele chochote katika Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itafuata taratibu zote za utungaji wa Sheria Ndogo zinazoelekezwa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji).

Usimamizi wa Sheria Ndogo

7. (1)Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kutokuwa na kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha

zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4)Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri.

Uteuzi wa Wakala

8. Halmashauri inaweza kuteua Kampuni, Asasi au Taasisi yoyote kukusanya Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika vyanzo vilivyokubaliwa kukusanywa na Wakala.

Wajibu wa Wakala

9. Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya au kupokea Ushuru katika eneo na chanzo alichopangiwa kwa viwango vilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya Mkataba wa Uwakala kati yake na Halmashauri;

(c) kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kuanza makusanyo ambapo dhamana hiyo itarejeshwa mwisho wa mkataba.

Uwezo wa afisa mwidhiniwa

10. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa :-

(a) kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kukusanya ushuru;

(b) kukagua eneo au chombo chochote atakachokitilia mashaka kuwa kinahifadhi au

kusafirisha bidhaa au kinatumika kukwepa kulipa ushuru ; na

(c) kufunga biashara au jengo lolote ambalo mmiliki wake atashindwa au kukataa kulipa Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA III

MAKOSA NA ADHABU

Makosa

11. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(1) Kwa Wakala yeyote;

(a) kukusanya ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba kutoka kwa Halmashauri;

(b) kukusanya au kujaribisha kukusanya ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo hizi;

(c) kushindwa kuwasilisha au kuwasilisha kiwango pungufu ya kiwango cha ushuru alichokubaliwa

katika mkataba;

(d) kukusanya ushuru kwa mbinu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri.

(2) Kwa mtu yeyote endapo;

(a) atashindwa, atadharau, au atakaidi au atakataa kulipa Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ushuru;

(c) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; na

(f) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na

mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne(24) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufililisha kosa

13. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoekelezwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa Tangazo la Serikali Na. 381 la mwaka, 2011,

Tangazo la Serikali Na. 343 la mwaka 2014 na sehemu ya Tangazo la Serikali na 376 la mwaka 2011

14. 1. Sheria Ndogo hizi zinafutwa;

(a) Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2011,

(b) Sheria Ndogo za (Ada na ushuru) (Marekebisho) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2014,

2. Jedwali la nne la Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha magari) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2011 zinafutwa

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA
*(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 4(1)*

1. ADA ZA HUDUMA ZA ARDHI

*(i) Vibali vya ujenzi*

| Na | Kibali cha ujenzi | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Eneo la msingi lisilozidi mita za mraba 50 | 25,000/= |
| 2. | Eneo la msingi linalozidi mita za mraba 51 lakini lisilozidi mita za mraba 60 | 38,000/= |
| 3. | Eneo la msingi linalozidi mita za mraba 61 lakini lisilozidi mita za mraba 250 | 50,000/= |
| 4. | Eneo la msingi lin alozidi mita za mraba 251 lakini lisiloz idi mita za mraba 350 | 63,000/= |
| 5. | Eneo la msingi linalozidi mita za mraba 351 lakini lisilo zidi rnita za rnraba 600 | 100,000/= |
| 6. | Eneo la msingi linalozidi mita za mraba 60l lakini lisilozidi mita za mraba 900 | 135,000/= |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Eneo la msingi linalozidi rnita za mraba 901, kwa kila mita ya rnraba inayozidi | 1,500/ |
| | (a) msingi wa zaidi ya ghorofa mbili kwa mita ya mrnba. | 1,725/= |
| | (b) jengo la kawaida | 1,950/= |
| | (c ) msingi wa kiwanda kidogo kwa kila mita ya mraba | 1,725/= |
| | (d)Viwanda vikubwa | 2,850/= |
| 8. | Ada ya ujenzi wa ghala kwa kila mita ya mraba | 2,000/= |
| 9. | Mnara (installation fees) | 2,500,000/= |
| 10 | Kupitisha marekebisho ya ramani | 50% ya gharama zilizolipiwa awali |
| 11 | Ongezeko na marekebisho ya jengo lililopo kwa mita ya mraba | 2,000/= |
| 12 | Ujenzi wa uzio wa mita 20 kwa kila enco kwa kila mita moja kwa miezi sita | 600/= |
| 13 | Kwa kila mwezi unaoongczeka kwa mita | 750/= |
| 14 | Kwa kipindi kinachozidi miezi 20 au sehemu kwa mita | 600/= |
| 15 | Ujenzi wa uzio wa kudumu | 1,000/= |
| 16 | Pale ambapo thamani ya jengo haiziadi sh.3,000,000/= | 45,000/= |
| 17 | Pale ambapo thamani ya jengo haizidi sh.3,000,000/= lakini haizidi 15,000,000/= | 135,000/= |
| 18 | Pale ambapo thamani ya jengo inazidi sh. 15,000,000/= lakini haizidi 30,000,000/= | 202,500/= |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 19 | Pale ambapo thamani ya jengo inazidi 30,000,000/= | 337,500/= |
| 20 | Ada ya maombi ya uwekaji wa bango | 100,000/= Kwa kila kibali |
| 21 | Ada ya matumizi ya jengo | 50% ya Ada ya kibali |

(ii) Ada na Vibali vya kubadilisha matumizi ya Ardhi, kugawa viwanja, mashamba au kurekebisha mchoro

| | Matumizi ya Awali | Matumizi yanayoombwa | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|---|
| 1 | Makazi pekee | Makazi na biashara | 80,000/= |
| 2 | Makazi pekee | Makazi zaidi ya moja | 100,000/= |
| 3 | Makazi pekee | Shule,Hosteli,Zahanati na huduma nyinginezo za jamii | 200,000/= |
| 4 | Makazi pekee | Hoteli | 200,000/= |
| 5 | Makazi na biashara | Kituo cha mafuta | 250,000/= |
| 6 | Makazi na biashara | (Maduka makubwa ) Super Market/Shooping Mall | 300,000/= |
| 7 | Makazi pekee | (Viwanda/huduma) Service Trade/Industrial | 200,000/= |
| 8 | Makazi pekee | Ghala (Yard/Godown) | 200,000/= |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | Biashara | Makazi | 100,000/= |
| 10 | Kugawa shamba kuwa viwanja vya makazi | makazi | 100,000/= |
| 11 | Kugawa kiwanja cha makazi | makazi | 100,000/= |
| 12 | Kugawa kiwanja kwa matumizi ya hoteli | biashara | 200,000/= |
| 13 | Kugawa kiwanja kwa matumizi ya shule, hosteli, zahanati na huduma nyinginezo za jamii. | biashara | 100,000/= |
| 14 | Ada ya uhakiki wa umiliki kiwanja au shamba (Official Search) | Matumizi yoyote | 50,000/= |

3. ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| Na | Aina ya mali | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1 | Kukodisha ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya semina au shughuli binafsi | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| 2 | (a) Kupanga kizimba cha biashara sokoni | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| | (b) Kupanga chumba au kibanda eneo la kituo cha mabasi (stendi yoyote). | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| | (c) Kupanga chumba cha soko lolote la Halmashauri | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| | (d) Kupanga au kuweka kontena mwavuli au uwazi wa kuuuzia vitu kama vile mbao au eneo lolote la wazi. | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| 3 | Kukodi majengo mengine ya Halmashauri | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| 4 | Kukodi magari ya Halmashauri ya Jiji | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| 5 | Kukodi Genereta | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| 6 | Kukodi mitambo na mashine nyingine yoyote ya Halmashauri | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| 7 | Kodi ya gardeni ya Halmashauri iwapo kuna shughuli maalumu. | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |
| 8 | Kukodi ardhi ya Halmashauri kwa matumizi maalum | Kwa mujibu wa bei ya soko ya wakati huo |

4. ADA YA UPIMAJI WA AFYA

| Ada husika | Kiwango cha Ada |
|---|---|
| 1. Homa ya manjano katika masaa ya kawaida; | |
| (a) Raia | 7,000/= |
| (b) Mgeni | 10,000/= |
| (c)Vipimo vya afya kwa watumishi wa hoteli, bucha na maduka kila baada ya miezi sita | 1,500/= |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

| | |
|---|---|
| (d) Udhibiti wa wadudu waharibifu kwenye makazi ya kawaida (Kwa mita ya mraba) | 1,500/= |

5. ADA ZA UWEKAJI UZIO KWENYE ENEO LA UJENZI

| Na | MUDA | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa uzio kwa mita 20 kwa kila eneo la mita moja kwa miezi sita | 1,500/= |
| 2 | Kwa kila mwezi unaoongezeka kwa mita | 2,000/= |
| 3 | Kwa kipindi kianachozidi miezi 20 au sehemu kwa mita | 3,000/= |

6. USHURU WA MACHINJIO

| Na | Mnyama | Kiwango cha ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2000/= | Kila ng'ombe mmoja |
| 2. | Mbuzi na kondoo | 1000/= | Kila mbuzi au kondoo mmoja |
| 3. | Nguruwe | 2000/= | Kila nguruwe mmoja |

7. USHURU WA KULAZA MIFUGO KWENYE MAENEO YA MACHINJIO IKIWA INASUBIRI KUCHINJWA

| Na | Mfugo | Kiwango cha Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 1000/= | Kila ng'ombe mmoja |
| 2. | Mbuzi, kondoo | 500/= | Kila mbuzi au kondoo mmoja |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Nguruwe | 500/= | Kila nguruwe mmoja |

8. USHURU WA UKAGUZI WA AFYA YA MNYAMA KABLA HAJACHINJWA

| Na | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 500/= | Kwa kila mnyama |
| 2. | Mbuzi, kondoo | 250/= | Kwa kila mnyama |
| 3. | Nguruwe | 500/= | Kwa kila nguruwe |

9. USHURU WA UKAGUZI WA NYAMA ILI KURUHUSU KWENDA BUCHANI

| Na | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 1500/= | Kwa kila mnyama |
| 2. | Mbuzi,kondoo | 250/= | Kwa kila mnyama |
| 3. | Nguruwe | 500/= | Kwa kila nguruwe |

10. ADA NA USHURU WA KUINGIZA WANYAMA NA NYAMA ILIYOCHINJWA NJE YA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA

| Na | Aina | Kiwango cha Ada/ Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuingiza nyama yoyote | 100/= kwa kg 1 | Kwa kila mnyama |
| 2. | Kuingiza wanyama wa kufuga Ng'ombe, Punda na Farasi | 10,000/= | Kwa kila mnyama |
| 3. | Kuingiza Nguruwe | 5,000/= | Kwa kila nguruwe |

11. HUDUMA NYINGINE ZINAZOHUSU MIFUGO

| Na | Aina ya mfugo | Kiwango |
|---|---|---|

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kuanzisha josho la mifugo | 30,000/= @kila josho |
| 2. | Ada na ushuru wa usafirishaji wa ngozi | 200/= Ng'ombe<br><br>100/= Mbuzi/Kondoo |

12. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na | Ukubwa wa gari | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Gari tani 1 | 2000/= Kwa Safari(trip) |
| 2 | Gari tani 2 | 2000/= Kwa Safari(trip) |
| 3 | Gari tani 3 | 2000/= Kwa Safari(trip) |
| 4 | Gari tani 4-6 | 3000/= Kwa Safari(trip) |
| 5 | Gari tani 7 | 5000/= Kwa Safari(trip) |
| 6 | Gari tani 8 na kuendelea | 10,000/= Kwa Safari(trip) |
| 7. | Kibali cha kuchimba madini ya ujenzi | 50,000/= |

13. ADA NA USHURU UTOKANAO NA BURUDANI ZA MICHEZO

| *Na* | *Tukio la Burudani* | *Kiwango cha Ada/ Ushuru* |
|---|---|---|
| *1* | Uimbaji kwenye tamasha | 100,000/=kwa tamasha |
| *2* | Uimbaji wa kongamano | 80,000/kila kongamano |
| *3* | Usajili chama cha Baiskeli na Pikipiki | 70,000/= kwa usajili |
| *4* | Usajili wa vikundi vya sanaa au kwaya | 50,000/= kwa usajili. |
| *5* | Usajili wa vyama vya michezo na vilabu | 70,000/= kwa usajili. |
| *6* | Usajili wa vibanda vya filamu | 70,000/= kwa usajili |
| 7 | Kibali cha kuchezesha disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho (Sinema, video, maigizo, sarakasi. | 100,000/= Kwa tukio |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 8 | Ada ya kutangaza burudani | 80,000/= kwa kibali |
| 9 | Kibali cha kuchezesha Michezo ya Kubahatisha kwa kutumia mashine. | 300,000/= Kwa kibali kwa mwaka |
| 10 | Kibali cha mchezo wa pool table | 100,000/=kwa mwaka. |
| 11<br><br>12<br><br>13 | kibali cha tamasha la maonesho<br><br>Bahati nasibu ndogo ndogo (fete)<br><br>Kibali cha matangazo | 100,000/= kwa onesho<br><br>100,000/= kwa mchezo<br><br>100,000/= kwa tangazo ya biashara. |
| 14 | Washereheshaji | 50,000/= kwa tukio |
| 15 | Wapambaji wa kumbi za burudani ( harusi, sherehe za jikoni, sherehe za kuaga binti na nyinginezo) | 50,000/= kwa tukio |
| 16 | Mtoa burudani (d.j) | 50,000/= kwa tukio |
| 17 | Wamiliki wa kumbi mbalimbali | (i) Ukumbi unaochukua watu 100-200 shilingi 30,000/=kwa kila tukio<br><br>(ii) Ukumbi unaochukua watu 300-500 shilingi 40,000/= kwa kila tukio |
| 18 | Wapishi wa vyakula | 50,000/= kwa tukio moja kwa siku |
| 19 | Picha jongevu na mnato | 30,000/= kwa tukio moja kwa siku. |
| 20 | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei (promotion) | 40,000/= kwa tangazo |
| 21 | Maombi ya kibali cha kufanya Tiba za Jadi | 20,000/= kwa siku |
| | | |

14. USHURU WA MAZAO YA KILIMO

| Na. | Aina ya Mazao | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mazao ya biashara na Chakula | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

## 15. USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Na. | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Aina zote za mazao ya Misitu | Asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia |

## 16. ADA NA USHURU KUTOKANA NA HUDUMA ZINGINE

| Na | Aina ya ada/ Ushuru | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya utambulisho (stika za Halmashauri) kwa ajili ya vyombo vya huduma ya usafiri bodaboda, bajaji, guta, tax, na daladala | 20,000/= kwa kila stika (itadumu kwa mwaka mmoja) |
| 2. | Ada ya kibali cha kununua mazao | 100,000/= kwa kila kibali na kitadumu kwa mwaka mmoja. |
| 3 | Ada na ushuru wa vibanda vya huduma za fedha kupitia simu za mkononi | 80,000/= kwa mwaka |
| 4 | Ada ya kibali cha night club | 300,000/= kwa mwaka |
| 5 | Ada na kibali cha kumbi za vikao na starehe zingine | 100,000/=kwa mwaka |
| 6 | Ada ya maombi ya kibali cha mziki | 100,000/= kwa siku |
| 7 | Ada ya maombi ya kibali cha tangazo la biashara | 100,000/= kwa masaa nane |
| 8 | Ada ya kibali cha mambo mengine ya kiutamaduni | 100,000/= kwa mwaka |
| 9 | Ada ya maombi ya kibali cha tangazo la sherehe harusi | 100,000/= kwa siku |
| 10 | Ada ya kusajili timu ya mchezo | 80,000/= kwa kila usajili |
| 11 | Ada ya kibali cha mchezo wa magari au pikipiki | 100,000/= kwa masaa sita |
| 12 | Ushuru wa pombe za kienyeji | 500/= kwa kila plastic |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

17. USHURU WA MAEGESHO MAALUM (RESERVED PARKING)

| Na | Aina | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Basi la abiria zaidi ya 40 | 1000/= kwa siku |
| 2 | Basi la abiria chini ya 40 | 1,000/=kwa siku |
| 3. | Basi abiria chini ya 20 | 1,000/= kwa siku |
| 4. | Lori la uzito chini ya tani 10 | 1,000/= kwa siku |
| 5. | Lori la uzito zaidi ya tani 10 | 1,000/= kwa siku |
| 6. | Gari ndogo lisilozidi tani 3 | 1000/= kwa siku |
| 7. | Gari ndogo lisilokuwa la mizigo | 1,000/= kwa siku |
| 8. | Pikipiki | 1,000/= kwa siku |
| 9. | Bajaji | 1,000/= kwa siku |
| 10. | Magari mengine yasiyo ya biashara | 1,000/= kwa siku |

18. ADA YA SEHEMU YA KUOSHA MAGARI

| Na | Aina ya shughuli | Ushuru kwa mwezi |
|---|---|---|
| 1. | Sehemu zote za kuosha magari zenye leseni | Tshs. 80,000/= |

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA PILI
(*Limetungwa* c*hini ya Kifungu cha 13*)
HATI YA KUKIRI KOSA

Mimi ………………………………………………… nakiri mbele ya ………………………………………………… ambaye ni Mkurugenzi, kwamba, mnamo tarehe ……. ya mwezi ……… mwaka ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………… cha Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kwa hiyari yangu niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru unaodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe …… ya mwezi …………… mwaka …………
Jina……………………..…………………………
Saini……………

Mbele ya:
Jina……………………………………………….
Cheo ……………………………………………..
Saini ………………

*Tangazo la Serikali Na.909 (Linaendelea.)*

Muhuri wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya Umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio la kikao cha Mkutano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 10/06/2020 na kubandikwa mbele ya;

SAAD A. MTAMBULE

KAIMU MKURUGENZI

*HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA*

GIBSON J. MWAKALIBULE

MWENYEKITI WA MKUTANO

*HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA*

NAKUBALI

DODOMA
05/08/2020

SELEMANI S. JAFO
*WN OR-TAMISEMI*
DODOMA